# UTARATIBU WA HUDUMA ZA MAABARA

1. Huduma za Maabara zinatolewa saa 24 kila siku.
2. Mgonjwa/Mteja anayehitaji huduma za uchunguzi ataelekezwa sehemu ya kusubiria na kupewa mwongozo kuhusu utaratibu wa namna ya kuingia kuchukuliwa vipimo/sampuli na Mhudumu wa Maabara (Mgonjwa ataingia kwa kufuata namba zinazotolewa na Mhudumu wa Maabara).
3. Mgonjwa/ mteja atapokelewa na mtaalam wa maabara eneo la mapokezi kwa ajili ya kuhakiki taarifa zilizojazwa kwenye fomu ya maombi ya vipimoau kwenye mfumo wa kompyuta wa utunzaji kumbukumbu (INAYA).
4. Mgonjwa ataelekezwa kuelekea kwenye chumba cha kuchukulia vipimo kwa ajili ya huduma husika (Wagonjwa waliozidiwa na wenye mahitaji maalum hupewa kipaumbele).
5. Mtaalam wa Maabara atatoa maelekezo kwa kila mgonjwa kuhusu aina ya kipimo, namna ya kumchukua mgonjwa kipimo na muda utakaotumika kukamilisha uchunguzi.
6. Jina na nambari ya utambulisho wa mgonjwa vitaandikwa kwenye chombo cha kuhifadhia sampuli ya mgonjwa kabla ya kuweka sampuli kwenye chombo husika kwa ajili ya kumbukumbu sahihi.
7. Sampuli itachukuliwa kwa mgonjwa kwa kiwango cha kutosha na itahifadhiwa kwenye chombo cha kuhifadhia sampuli. Sampuli za wagonjwa waliolazwa zitachukuliwa na wauguzi na zitaletwa maabara kwa ajili ya uchunguzi kwa kufuata mwongozo.

8. Sampuli zilizochukuliwa na taarifa binafsi za mgonjwa zitafanyiwa uhakiki mapokezi kabla ya kupelekwa eneo la ndani (maabara) kwa ajili ya uchunguzi.
9. Taarifa za kila sampuli zitaingizwa kwenye mashine kabla ya sampuli kupimwa ili kuhakikisha majibu sahihi yanatolewa kwa kila mgonjwa.
10. Vipimo vitafanyika kwa kufuata miongozo mbalimbali iliyoandaliwa na wataalam wa Maabara.
11. Majibu yote ya vipimo yanafanyiwa uhakiki na kurekodiwa kwenye rejesta za maabara kabla ya kurejeshwa kwenye maeneo mbalimbali ya Taasisi wanapohudumiwa wagonjwa husika.
12. Vipimo vinavyohitaji majibu ya dharura vinapewa kipaumbe ili kuwezesha matibabu ya haraka kwa wagonjwa waliozidiwa (Majibu haya hutolewa ndani ya saa moja baada ya sampuli kupokelewa na majibu mengine hutolewa ndani ya masaa manne baada ya kupokea sampuli).
13. Sampuli zote zenye mapungufu mbalimbali zinabainika katika hatua za awali ili kuwezesha utatuzi wa tatizo mapema.